

USAFIRI WA UMMA

Mabasi yatua, miundombinu ikiharibika

Nasra Abdallah, Mwananchi
nabdallah@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Awamu ya kwanza ya mabasi yaendayo haraka yatakayotoa huduma katika awamu ya pili ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) yamewasili nchini, huku baadhi ya miundombinu ikiwa haijakamilika na mengine ikianza kuharibika.

Mabasi hayo 99 ya Kampuni ya Mtanzania, Mofat, ni sehemu ya yale 250 yatakayotoa huduma katika njia hiyo, huku mengine yakitarajiwa kuwasili mwisho wa Agosti mwaka huu, tayari kuwahudumia Watanzania.

Mabasi hayo yamewasili kutoka China yalikotengenezwa, na taarifa ambazo *Mwananchi* limedokeza ni kwamba yaliwasili tangu Agosti 5, na kuanza kupakuliwa kutoka melini katika Bandari ya Dar es Salaam.

Njia yatakayotoa huduma mabasi hayo, inahusisha barabara ya Mbagala hadi Gereza yenye urefu wa kilomita 20.3, iliyojengwa na Kampuni ya Sinohydro kutoka China, na ilikabidhiwa kwa DART tangu Agosti 2023.

Katika awamu hiyo, kampuni ya Mofat ndiyo imepewa mkataba wa miaka 12 kutoa huduma hiyo, na mabasi yake yatatumia nishati ya gesi asilia.

Kutokana na hatua hiyo yenye matumaini kwa wakazi wa Mbagala

la na wanaotumia njia hiyo, *Mwananchi* jana, ilitembelea miundombinu yatakopopita mabasi hayo kujionea hali halisi. Baadhi ya maeneo yalikutwa hayajakamilika yakiendelea na ujenzi na mengine kuharibiwa.

Maeneo ambayo ujenzi wake unaonekana kuendelea ni kipande cha barabara ya mabasi hayo maeneo ya Kamata, Kariakoo, ambako walishuhudiwa mafundi wakien-delea na kazi.

Pia, miundombinu mengine ambayo bado haijakamilika ni ya mageti janja kwa ajili ya abiria kuingia ndani ya vituo kwa kutumia kadi na siyo tiketi.

Katika hili, *Mwananchi* ilipita katika vituo hivyo kuanzia Kamata hadi Mbagala Rangi Tatu, hakuna hata kimoja ambacho tayari kimefungwa mageti hayo.

Aidha, katika uharibifu wa miundombinu, baadhi ya taa za kuongozea magari zimeharibika na nyingine nguzo zake kuanguka.

Pia, taa nyingine zimevunjwa, jambo linalochangiwa na kupita kwa magari ya mizigo kutoka bandarini.

Walichosema DART

Wakati hali ikiwa hivyo, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Dk Athuman Kihamia, alikiri miundombinu hiyo kutokamilika na kueleza kuwa kwa eneo la Kamata, mabasi hayo



Eneo la Kamata jijini Dar es Salaam, ambako miundombinu ya kupita mabasi ya mwendokasi ikiwa bado kwenye matengenezo. Picha Nasra Abdallah



Hivyo kazi hii itakopokamilika ni matumaini yetu kabla ya mwezi huu haujaisha basi yawe yameanza kutoa huduma barabarani."

Mtendaji Mkuu DART, Dk Athuman Kihamia

yatapita yanapopita magari mengine kwa sasa mpaka hapo ujenzi utakopokamilika.

"Kutokamilika kwa kipande kile hakuna athari kwa kuwa ni padogo tu, hivyo na hayo mabasi yatapita kunapopita magari mengine kwa sasa. Si umeona licha ya ujenzi huo kuendelea, gari zinapita kama kawaida, basi na yenyewe yatapita humo," alisema Dk Kihamia.

Kuhusu kutofungwa kwa mageti janja, alisema kazi hiyo inatarajiwa kuanza mwezi ujao na kwa sasa kitakachofanyika ni abiria kutumia tiketi kwa muda wa mpito.

"Ni kweli mageti janja bado hayajafungwa. Tunategemea kazi hiyo itaanza mwezi ujao, lakini hii haiwezi kuwa sababu mabasi hayo kutoanza kutoa huduma, kwani tumeona abiria waanze kutumia tiketi kwa kipindi cha mpito," alisema mtendaji huyo.

Kuhusu gesi, alisema kuna kituo cha kujazia ndani ya kituo kikubwa cha mabasi hayo cha Mbagala, hivyo suala la gesi halitasumbua.

Alipoulizwa ni lini hasa mabasi hayo yataanza kazi, alisema lengo ni ndani ya mwezi huu kwa kuwa bado hayajamaliza kupakuliwa bandarini, hivyo ni vigumu

kuahidi.

"Unajua licha ya kazi ya kuyapakua kwenye meli mabasi hayo kuanza tangu juzi, kazi hiyo inaendelea hadi ninavyozungumza na wewe hapa, na tumelazimika kuyaomba kibali cha dharura kwa kuwa wananchi wameshayasubiria sana.

Kuhusu madereva waliokidhi vigezo vya kuendesha, alisema wapo 150 tayari kuingia barabarani na kazi hiyo ya kuwasili iliachwa Mamlaka ya Usafiri Ardhi (LATRA), Jeshi la Polisi wa Usalama Barabarani na Chuo cha Usafirishaji (NIT).

Maoni ya wananchi

"Kufika kwa mabasi ni jambo moja, lakini kuanza kutoa huduma ni jambo jingine, kwani hii siyo mara ya kwanza kuahidiwa. Labda tutaamini pale tutakapoyaona barabarani," alisema Shabani Juma.

Ally Biasi alisema magari hayo yaki-anza kazi wananchi wataweza kutoka na kurudi majumbani kwao kwa wakati, huku akiwataka wasimamizi wa mradi huo kuhakikisha abiria wanapata usafiri huo kwa muda na si kukaa muda mrefu vituoni.

The Citizen Friday August 8, 2025 Pg 2 Dart confirms arrival of 99 BRT buses



BRT buses belonging to local operator Mofat Company Limited at the Dar es Salaam port. PHOTO | COURTESY

By Hellen Nachilongo

@musanachi60

hnachilongo@tz.nationmedia.com

Dar es Salaam. The government has confirmed the arrival of 99 long-awaited buses for Phase II of the Bus Rapid Transit (BRT) which is scheduled to start operating next month.

The 20.3-kilometre Phase II route, constructed by China's Sino-hydro Construction Limited, cost a total of \$159.32 million (Sh285.1 billion), and connects Mbagala to the city centre.

It also connects with the Phase I

at Gerezani area in Kariakoo.

Speaking to *The Citizen* yesterday Dar es Salaam Rapid Transit Agency (Dart) chief executive officer, Dr Athumani Kihamia, confirmed that the vessel carrying the 99 buses docked at the Dar es Salaam Port on the night of August 5, 2025 and are currently being cleared.

"The buses have been offloaded, but are yet to leave the port. An additional 52 buses are expected to arrive on August 26 or 27, bringing the total to 151 buses set to oper-

ate along the Phase II route," Dr Kihamia said.

He noted that the newly arrived units, 18-metre-long articulated buses manufactured by Golden Dragon, are designed specifically for the BRT trunk route and will significantly boost transport capacity once deployed.

"These are just the initial units. Eventually, the route will require a total of 755 buses for full operation," he added.

Dr Kihamia revealed that the buses were shipped from the Glovis Precious Port in Xiamen, China, where he personally witnessed the loading process on July 17.

Local operator

The buses belong to local operator Mofat Company Limited, which has been contracted to run part of the BRT rote.

In preparation for the operational rollout, Mofat launched a recruitment drive on June 21 aimed at creating over 1,000 job opportunities.

As of June 23, the company's chief operations officer, Mr Mabrouk Masasi, confirmed that 423 vacancies had already been announced.

"We've begun recruiting 423 employees, 255 drivers and 158 station assistants, with the remainder being mechanics and support staff," Mr Masasi said.

He added that more vacancies would be advertised once operations commence, with the total workforce expected to reach around 1,100 employees.

"The first batch of buses is set to begin operations on September 1, 2025. Our preparations include receiving and installing electronic gate systems, training staff, and finalising the fare collection infrastructure," he said.

All incoming buses will be stationed at the Mbagala terminal ahead of deployment.

FORM 58

IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE

AT ONE STOP CENTRE

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.

16620 OF 2025.

In The Matter Of The Estate Of The Late

AMANI STUART CHITEMO.

AND

In the matter of application for letters of Ad-

ministration By HELLEN AGREY NDOMONDO.

GENERAL CITATION

(Rule 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 26TH day of AUGUST, 2025.

Dated at DAR ES SALAAM this 7TH Day of AUGUST, 2025.

Senior Resident Magistrate.